

Mamlaka Yetu Kanisani (Our Authority In Church)

Na

John Kombo

Mamlaka Yetu Kanisani (Our Authority In Church)

Na

John Kombo

September 10, 2014

Mamlaka Yetu Kanisani

Sio kinachoonekana bora

Katika kila kujifunza neno la Mungu kunapaswa kuwa na viwango vya mamlaka. Maswali yote lazima yawe na vyanzo muhimu ya majibu. Sote tunapaswa kuwa na mamlaka ambayo tunategemea ili kuwa sahihi. Kwa sababu somo letu ni la kidini, sasa tunauliza, “MAMLAKA YETU NI YAPI KATIKA SOMO LA JINSI KANISA LIPASWA LIWE? VIWAPI VIPI VITAKAVYOTUMIKA ILI KUWA DHAHIRI KWAMBA MASWALI YATAPEWA MAJIBU SAHIHI?” Leo baadhi ya watu watasema kwamba kila mtu anaachwa kuchagua kilicho chema katika maswala yanayohusu dini. “Unaweza kufanya tu kilicho bora,” watu hao husema. “Kila mtu katika kiwango chake”. Biblia inasema kwamba, “*Ee BWANA najua ya kuwa njia ya mwanadamu haimo katika nafsi yake, kuelekeza hatua zake si katika uwezo wa mwanadamu.*” (Yer. 10:23). “*Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti.*” (Mit. 14:12). YESU ALISEMA, “*Wananiabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.*” (Mat. 15:9). Tunaweza kujifunza na kuona hilo, katika swala lolote la kidini, mawazo ya mwanadamu haina mamlaka.

Siyo kile ambaccho wengine hufanya

Imani ya pili katika mamlaka ya kidini ni kwamba kile kinachofanywa na wingi wa watu lazima liwe sahihi. Wale wanaoamini katika mipango fulani au tendo la kanisa watajisifu kuhusu ni watu wangapi wamekubali kufuata mipango yao au yale wanayofanya (wale wanaotumia vikombe vingi wanajisikia vivyo hivyo. Wana wafuasi wengi). Wazo hili halipo sahihi hasa kulingana na mamlaka ya dini yanavyokwenda. Yesu aalisema wengi wana dhani wako sahihi, lakini hawatambui (Mat. 7:22). Wengi wanafuata katika njia zisizo sahihi, lakini wachache wanaofuata ukweli (Mat. 7:13-14). Tunaweza kujifunza somo kutoka kwa Waisraeli waliohitaji mfalme ili afanane na nchi zilizowazunguka. Kwa kujaribu kuwa kama wengine walikataa mpango wa Mungu kuwa tawala (1 Sam. 8:5-7). Hivyo hili ni onyo kwa kanisa la Bwana wasijaribu kuwa kama madhehebu yanayoizunguka. Kama kanisa la Bwana wetu, tumeitwa kutoka kwao (2 Kor. 6:17). Sisi ni wateule (1 Pet. 2:9). Tatizo ni kwamba waumini dhaifu wa kanisa la Bwana wameruhusu uharibifu katika makusanyiko yao, n.k. vyombo vya muziki, vikombe vingi katika meza ya Bwana na wanawake wahubiri, n.k.

Ni Agano Jipya pekee

Kiwango pekee cha kweli ya mamlaka katika dini ni Agano Jipya. Tuna katekizimu, kitabu cha maombi, au muongozo wa sala kama mamlaka ya dini lakini hivyo siyo viwango vya dini. Yesu ana mamlaka yote mbinguni na duniani (Mat. 28:18). Alituma Roho Mtakatifu kwa mitume ili kuwaongoza katika kweli (Yoh. 16:13). Kila kilichoandikwa katika maandiko kimevuviwa na Mungu na inafaa katika matendo mema ya Wakristo (2 Tim. 3:16-17). Hatupaswi kuondoa au kuongeza katika kitabu cha Mungu (Ufu. 22:18-19). Sisi sote, ili tukubaliwe mbinguni lazima tukae katika mafundisho ya Kristo na tusiende zaidi ya hayo (2 Yoh. 9-10). Mwanadamu hapaswi kubadilisha wala kupotosha Injili (Gal. 1:7-9). Ni mhimu kuelewa kwamba Agano la Kale sio mamlaka ya Wakristo. Ilikuwa tu kiongozi hadi imani katika Kristo ilivyo kuja, lakini sasa wanadamu hawako tena chini ya kiongozi (Gal. 3:24-25). Sheria iliondolewa na kugongomewa katika jipya na agano bora, Agano Jipya la Bwana wetu Yesu Kristo (Ebr. 8:6-13)

Hivyo basi, wale wanaotii mamlaka ya Mungu mara zote watafundisha kile ambacho Biblia inafundisha na kukataa kufundisha chochote ambacho maandiko hayajaamuru. Watu wa Mungu wanapaswa kunena pale ambapo Biblia inanena na kunyamaza pale ambapo Biblia imenyamaza.

Ndg. John Kombo

Kanisa la Kristo Baruti

Nakuru, Kenya

